

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUCHOSA



Unapojibu tafadhari taja:
Kumb. Na. AB.208/117/01/61

- Tarehe 25 Mei, 2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa anapenda kuwatangia watazania wote kuwa Ofisi imepokea kibali cha Ajira Mbadala kutoka kwa Katibu Mkuu **OR-UTUMISHI** chenye Kumb. Na. FA.97/228/01/9 cha tarehe 13/05/2022 kwa ajili ya kujaza nafasi za kazi ya Katibu Mahsusii III na Mtendaji wa Kijiji III kwa masharti ya Kudumu. Hivyo Watazania wote wenye sifa mnakaribishwa kutuma maombi ya kujaza nafasi hizo kama ifuatavyo:

1. KATIBU MAHSUSI DARAJA LA III – NAFASI TATU (3)

i. Sifa za Kitaaluma kwa mwombaji:

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha IV waliohudhuria Mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihiani wa Hatua ya Tatu. Wawe wamefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja na wawe wamepata mafunzo ya Kompyuta kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata Cheti katika Programu za Windows, Microsoft Office, Internet, E-mail na Publisher.

ii. Majukumu ya Kufanya:

- Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida.
- Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanpoweza kushughulikia.
- Kusaidia kutunza taarifa/ kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao.
- Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
- Kumsaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi.

f) Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wa kazi.

iii. **Masharti ya Ajira:** Ajira ya kudumu

iv. **Mshahara:** Ngazi ya mshahara ataanzia TGS B kwa mwezi.

2. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III – NAFASI NANE (8)

a) Kazi na Majukumu ya Mtendaji wa Kijiji:

1. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
2. Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika Kijiji.
3. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiji.
4. Katibu wa mikutano ya kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
5. Kutafsiri na kusimamia sera, sheria na taratibu.
6. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
7. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaalamu katika Kijiji.
8. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
9. Mwenyekiti wa kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji.
10. Kupokea, kusikiliza na katatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
11. Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji na
12. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

v. **Masharti ya Ajira:** Ajira ya kudumu

vi. **Mshahara:** Ngazi ya mshahara ataanzia TGS B kwa mwezi.

vii. **Masharti ya Jumla kwa waombaji**

- a) Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania.
- b) Waombaji wote wawe na umri wa kuanzia miaka 18 na wasizidi miaka 45.
- c) Waombaji wote lazima waambatishe wasifu binafsi (CV) zenye mawasiliano ya uhakika, anuani, barua pepe na namba za simu.
- d) Waombaji wote wanatakiwa kuwa na namba ya Utambulisho wa Uraia (National Identification Number) kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
- e) Waombaji wote waombe kwa kufuata masharti ya TANGAZO LA KAZI.
- f) Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma (Diploma/ Certificates), nakala ya vyeti vya kidato cha nne (IV) au sita (VI) kwa wale waliofikia kiwango hicho, vyeti

vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa ya kazi husika na picha (Pssport size) mbili za hivi karibuni na iandikwe kwa nyuma. Viambatisho hivyo vibanwe pamoja kuondoa uwezekano wa kudondoka au kupotea.

• **Transcripts, Testimonials, Provisional results, Statement of results na hati za matokeo ya kidato cha IV au VI havitaruhusiwa.**

- g) Kuwasilisha vyeti vya kughushi na maelezo mengine itasababisha kuchukuliwa hatua za Kisheria.
- h) Waombaji ambao ni Watumishi wa Umma wapitishie barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa Waajiri wao na Waajiri wajiridhishe ipasavyo.
- i) Waombaji ambao walistaafu kazi kwa sababu yoyote ile hawaruhusiwi kuomba nafasi hizi.
- j) Waombaji wote waandike namba zao za simu kwenye maombi yao kwa ajili ya mawasiliano.
- k) Waombaji waonyeshe wadhamini wawili na mawasiliano yao, anuani na namba za simu.
- l) Waombaji wenye vyeti vya Kidato cha Nne/ Sita na cheti cha Taaluma ambavyo vimepatikana nje ya nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) na Baraza la Elimu ya Ufundi la Taifa (NACTE)
- m) Barua ya maombi iandikwe kwa Kiswahili au Kiingereza.
- n) Watakao chaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 10/06/2022 saa tisa na nusu (9:30) Alasiri.

Maombi yote yatumwe kwa:

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa,
S. L. P. 44,
Buchosa – Sengerema.

au,

District Executive Director,
Buchosa District Council,
P. O. Box 44,
Buchosa – Sengerema.

NB: Tangazo hili linapatikana katika tovuti ya Halmashauri www.buchosadc.go.tz, na katika mbao za matangazo za Halmashauri.

Tangazo hili limetolewa na


Julius T. Mulongo

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
BUCHOSA

S.L.P 44, BUCHOSA-SENGEREMA, Simu +255 (026) 2963630, Nukushi +255 (026) 2963629,
Barua pepe: ded@buchosadc.go.tz, Tovuti: www.buchosadc.go.tz